



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



MWALIKO KWA WATAZAMAJI WA NDANI WA
UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iko kwenye mchakato wa maandalizi ya kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Mwezi Oktoba, 2020.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili Watazamaji wa Uchaguzi wanaotaka kutazama Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Kupitia tangazo hili, Tume inapenda kuzialika Taasisi/Asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama Uchaguzi Mkuu unaotegemewa kufanyika mwezi Oktoba, 2020.

Taasisi/Asasi zenye nia ya kutazama Uchaguzi Mkuu zinatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo **Foreign Affairs House, Mtaa wa Shabani Robert/Garden Avenue** kuanzia tarehe 28 Novemba, 2019 na mwisho wa kupokea maombi hayo itakuwa ni tarehe 31 Januari, 2020.

Aidha, maombi hayo pia yanaweza kutumwa Tume kupitia anuani ya Posta ifuatayo;

Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Foreign Affairs House,

Mtaa wa Shabani Robert/ Garden Avenue,

S.L.P 10923,

DAR ES SALAAM.

Barua ya maombi pamoja na mambo mengjne itatakiwa kuainisha mambao yafuatayo:-

- (i) Anuani kamili ya Taasisi husika;
- (ii) Mahali/sehemu ambapo Taasisi husika inafanya kazi;
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa hati ya Usajili;
- (iv) Sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji;
- (v) Idadi ya watu ambao Taasisi/Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao;
- (vi) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi/Asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili wa Taasisi/Asasi;
- (vii) Ikiwa Taasisi/Asasi inahusisha Watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania.
- (viii) Kuambatisha Nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi/Asasi husika; na
- (ix) Kuambatisha Nakala/kivuli cha Katiba ya Taasisi/Asasi husika.

Tume baada ya kupokea barua za maombi itazitaarifu Taasisi/Asasi husika iwapo zimekubaliwa au kukataliwa.


Dkt. Wilson M. Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

27 NOVEMBA, 2019



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL ELECTORAL COMMISSION



INVITATION FOR LOCAL OBSERVERS TO OBSERVE
THE GENERAL ELECTION, OCTOBER 2020

The National Electoral Commission expects to conduct the General Election in October, 2020.

The law gives the National Electoral Commission mandate to invite and accredit observers who intend to observe the electoral process. Through this advertisement, the Commission would like to extend invitation for applications from institutions/organizations which intend to observe the General Election.

Institutions/organizations which intend to observe the General Election are required to submit their applications at the National Electoral Commission Offices located at Foreign Affairs House, Shaban Robert/Garden Avenue Street, from 28th November, 2019 and deadline for receiving applications shall be on 31st January, 2020.

The applications can also be sent through the following Postal address:-

National Electoral Commission,
Foreign Affairs House,
Shaban Robert/Garden Avenue Street,
P.o.Box 10923,
DAR ES SALAAM


An application letter should include the following:-

- (i) Full address of the institution/organization;
- (ii) Physical address of the institution/organization;
- (iii) Activities performed by the institution/organization as specified in their registration documents;
- (iv) Names and telephone numbers of leaders of the institutions/ organizations;

- (v) Number of individuals from the institution/organization who will participate in the observation of the electoral process including their particulars.
- (vi) Areas in which the institution/ organization plans to conduct observation;
- (vii) In the event the institution/ organization has foreign employees, at least two must be Tanzanians;
- (viii) A copy of the registration certificate/ documents;
- (ix) A copy of the institutions/ organizations Constitution;

The commission will communicate the status of the approval to the respective institution/organization accordingly.

Issued by;


Dr. Wilson M. Charles
DIRECTOR OF ELECTIONS

27TH NOVEMBER, 2019